## 7.0 Wajibu wa Mahakama Katika Makubaliano ya Kukiri Kosa

- Mahakama haipaswi kujihusisha kwa namna yoyote ile wakati wa makubaliano haya. Mahakama itahusika baada ya pande zote mbili kukamilisha makubaliano na kuyaweka katika maandishi na kusaini.

- Mahakama inapaswa kujiridhisha kwamba makubaliano haya yamefanyika bila shuruti baina ya pande zote mbili.

- Iwapo mahakama itakataa makubaliano hayo, itataja sababu za msingi za kukataa makubaliano, hivyo basi pande zote mbili zinatakiwa zikae na kufanya upya makubaliano mengine.

- Mahakama ikikubali makubaliano hayo ina wajibu wa kusajili makubaliano hayo na yanakuwa yamefungwa rasmi na kuwa kumbukumbu za mahakama.

## 9.0 Matokeo ya Makubaliano ya Kukiri Kosa

i) Mwendesha mashtaka anaweza kupunguza makosa makubwa katika hati ya mashtaka na kuacha makosa madogo au kufuta kabisa makosa mengine ;

ii) Mshtakiwa anaweza kukiri kosa aliloshtakiwa kwa makubaliano ya kufutwa kwa makosa mengine;

iii) Mshtakiwa hatokuwa na haki ya kusikilizwa na mahakama yaani kupelekwa mahakamani na kutoa utetezi au ushahidi juu ya kosa hilo;

iv) Mshtakiwa hatokuwa na haki ya kukata rufaa kuhusu uendeshaji wa kesi yake isipokuwa anaweza kukata rufaa kupinga utaratibu uliotumika wakati wa kutolewa kwa hukumu;

v) Mshtakiwa naweza kuamriwa kurudisha au kulipa fidia ya vitu vilivyopatikana kwa njia ya uhalifu, au vilivyotumika wakati wa kutenda uhalifu.

## 10.0 Maombi ya Kutengua Makubaliano ya Kukiri Kosa

Mkurugenzi wa mashtaka au mshtakiwa kwa madhumuni ya kulinda maslahi ya haki anaweza kuwasilisha maombi katika mahakama iliyomtia hatiani mshtakiwa pale makubaliano ya kukiri yanapokuwa yamefanyika kwa udanganyifu. Maombi hayo yanapaswa kuwasilishwa ndani ya kipindi cha siku sitini (60) baada ya mshitakiwa kutiwa hatiani kutokana na makubalino ya kukiri kosa.

## 11. 0 Hitimisho

Makubaliano ya kukiri kosa yanatoa fursa kwa watuhumiwa ambao wapo tayari kukiri makosa kwa hiyari yao wenyewe kwa lengo la kumaliza shauri bila kupitia mlolongo mrefu na kuwawezesha kuendelea na shughuli za kukuza uchumi wa nchi.

Aidha kwa upande wa Serikali, makubaliano ya kukiri kosa yamepunguza gharama za uendeshaji mashauri mahakamani, mlundikano wa mashauri mahakamani na msongamano wa wafungwa na mahabusu gerezani.

---


**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



# MAKUBALIANO YA KUKIRI KOSA

# MAKUBALINAO YA KUKIRI KOSA

## 1.1 Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa.

Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu katika maboresho ya sheria.

## 2.0 Maana ya Makubaliano ya Kukiri Kosa

Ni makubaliano maalumu katika kesi ya jinai kati ya mwendesha mashitaka na mshtakiwa ambapo mshtakiwa anakubali kukiri kosa moja au zadi katika makosa aliyoshtakiwa nayo ili apate nafuu ya kupunguziwa adhabu au kufutiwa baadhi ya makosa katika shauri linalomkabili. Katika makubaliano haya, mshtakiwa pia anaweza kukubali kutoa ushirikiano kwa mwendesha mashtaka ambao utawezesha kupatikana kwa taarifa zinazohusiana na kosa hilo aliloshitakiwa nalo.

Mfumo huu wa makubaliano ya kukiri kosa umeanza rasmi nchini, mwaka 2019 kufuatia marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Aidha, makubaliano yoyote ya kukiri kosa hayawezi kufanyika bila kuwa na kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka,kukubali makubaliano hayo yafanyike.

## 3.0 Sheria Zinazosimamia Makubaliano ya Kukiri Kosa

### Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20

Sheria hii inaainisha utaratibu wa kufuatwa wakati wa kufanya makubaliano ya kukiri kosa na makosa yanaruhusiwa kisheria kuingiwa makubaliano. Pamoja na sheria hii, kuna Kanuni ambazo zimeandaliwa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa makubaliano ya kukiri kosa kuanzia watu wanaohusika na makubaliano, namna yanavyofanyika na jinsi ya kuyarasimisha makubaliano hayo.

## 4.0 Muda wa Kufanya Makubaliano ya Kukiri Kosa

Sheria inaruhusu makubaliano haya yafanyike muda wowote kabla ya mahakama kutoa hukumu.

## 5.0 Makosa Yasiyoruhusiwa Kufanyiwa Makubaliano ya Kukiri Kosa

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai pamoja na kuruhusu mfumo wa makubaliano ya kukiri kosa imeainisha pia kuwa si makosa yote ya jinai yanaruhusiwa kuingiwa kwa makubalino ya kukiri kosa. Makosa yafuatayo hayahusiki kutumiwa kwa mfumo wa makubaliano ya kukiri kosa;

**i) Makosa ya udhalilishaji wa kingono yenye adhabu ya kifungo cha zaidi ya miaka 5 au udhalilishaji wa mtu aliye chini ya umri wa miaka 18.**

**ii) Uhaini na makosa yanayohusiana na uhaini**

**iii) Ugaidi**

**iv) Kumiliki au kusafirisha dawa za kulevya zenye thamani ya zaidi ya milioni mia moja, kwa dawa za kulevya ambazo thamani yake haijathaminishwa iwapo ni;**

Sheria hii imempa Waziri mwenye dhamana na masuala ya sheria kutengeneza kanuni ambazo zinaweza kuongeza aina ya makosa mengine ambayo mfumo makubaliano ya kukiri kosa hautatumika.

## 6.0 Utaratibu wa Kufanya Makubaliano ya Kukiri Kosa

Mshtakiwa, wakili wake au mwendesha mashtaka wanaweza kuanzisha mchakato wa makubalino ya kukiri kosa na kuijulisha mahakama kabla ya hukumu. Kabla ya kuingia makubaliano ya kukiri kosa upande wa mashtaka utaazingatia masuala yafuatayo;

i). Mazingira ya utendakaji wa kosa;

ii). Taarifa/rekodi za kutiwa hatiani mshtakiwa;

iii). Hasara au uharibifu aliyosababishiwa mhanga;

iv). Maslahi ya jamii.

Makubaliano hayo yanatakiwa kuwa kwenye maandishi ikijumuisha taarifa zote muhimu zitakazojadiliwa katika kikao hicho. Makubaliano yatatakiwa kusomwa kwa mshtakiwa katika lugha atakayoweza kuelewa. Iwapo mshitakiwa alifanyiwa tafsiri ya makubaliano hayo kwa kutumia mtaalamu wa tafsiri, mtaalamu huyo atatakiwa kutoa uthibitisho kisheria kwamba ni mbobevu katika lugha hiyo, na ametoa tafsiri sahihi katika makubaliano hayo kwa mujibu wa maudhui husika

- Makubaliano hayo yatatakiwa kukubaliwa na mshtakiwa.

- Makubaliano hayo yatatakiwa kutiwa saini na mwendesha mashitaka, Mshtakiwa pamoja na wakili wake kama yupo (ushudiaji).